

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**MUHTASARI WA PATO LA TAIFA
ROBO YA KWANZA (JANUARI – MACHI), 2021
MWAKA WA KIZIO 2015**



**Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Wizara ya Fedha na Mipango
Julai, 2021**

Yaliyomo

Majedwali	3
Viambatisho.....	5
1.0 Utangulizi	6
1.1 Uchumi wa Dunia.....	6
1.2 Uchumi wa Nchi Zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara	6
1.3 Uchumi wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika	6
1.4 Ukuaji wa Uchumi Katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.....	7
1.5 Ukuaji wa Uchumi Nchini Tanzania	8
1.5.1 Ukuaji wa Uchumi Katika Robo ya Kwanza, Mwaka 2021	8
1.5.2 Mchango wa Shughuli Kuu za Uchumi, Robo ya Kwanza, Mwaka 2021.....	9
1.5.3 Viwango vya Ukuaji wa Shughuli za Kiuchumi, Januari Machi 2021	10
1.5.4 Mchango Katika Ukuaji wa Uchumi, Robo ya Kwanza, Mwaka 2021	10
2.0 Ukuaji wa Shughuli za Uchumi.....	11
2.1 Kilimo, Misitu na Uvuvi	11
2.1.1 Mazao	11
2.1.2 Mifugo	12
2.1.3 Misitu.....	12
2.1.4 Uvuvi	13
2.2 Uchimbaji wa Madini na Mawe	13
2.3 Viwanda.....	14
2.4 Umeme	14
2.5 Maji Safi na Maji Taka.....	14
2.6 Ujenzi	15
2.7 Biashara na Matengenezo.....	16
2.8 Uchukuzi na Uhifadhi wa Mzigo	16
2.9 Malazi na Huduma ya Chakula	16
2.10 Habari na Mawasiliano.....	17
2.11 Fedha na Bima.....	17
2.12 Upangishaji Majengo	18
2.13 Shughuli za Kitalaam, Sayansi na Ufundu	18
2.14 Huduma Zinazohusiana na Utawala.....	19
2.15 Utawala na Ulinzi	19
2.16 Elimu	20
2.17 Afya na Huduma za Jamii	20
2.18 Sanaa na Burudani.....	20
2.19 Huduma Nyingine za Kijamii.....	21
2.20 Shughuli za Kaya katika Kuajiri	21
3.0 Hitimisho	21

Majedwali

Jedwali Na 1: Uzalishaji wa Madini, Robo ya kwanza Mwaka 2016 – 202113

Vielelezo

Kielelezo 1: Ukuaji wa Uchumi Katika Nchi za SADC - Robo ya Kwanza, Mwaka 2021.....	7
Kielelezo 2: Ukuaji wa Uchumi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Robo ya Kwanza Mwaka	
2016 – 2021	8
Kielelezo 3: Kasi ya Ukuaji wa Pato la Taifa, Robo ya Kwanza Mwaka 2015 – 2021	9
Kielelezo 4: Mchango wa Shughuli Kuu za Kiuchumi, Robo ya Kwanza Mwaka 2021	9
Kielelezo 5: Ukuaji wa Shughuli za Uchumi - Robo ya Kwanza, Mwaka 2021	10
Kielelezo 6: Uzalishaji wa Baadhi ya Mazao, Robo ya Kwanza Mwaka 2020 – 2021	11
Kielelezo 7: Maji yaliyozalishwa (Mita za Ujazo Milioni), Robo ya kwanza, Mwaka 2017 – 2021 .	15
Kielelezo 8: Mauzo ya Huduma za Mawasiliano, Robo ya kwanza Mwaka 2017 – 2021	17
Kielelezo 9: Mikopo na Amana za Benki, Robo ya Kwanza Mwaka 2016 – 2021	18

Viambatisho

Kiambatisho Na.1: Pato la Taifa kwa Shughuli za kiuchumi kwa Bei za Mwaka 2015 – Sh. Milioni	23
Kiambatisho Na.2: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Bei za mwaka 2015 – Asilimia	25
Kiambatisho Na. 3: Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Bei za Soko (Bei za Miaka inayohusika) – Sh. Milioni	27
Kiambatisho Na. 4: Mchango wa Shughuli za Kiuchumi katika Pato la Taifa kwa Bei za Soko (Bei za miaka inayohusika) - Asilimia	29

1.0 Utangulizi

Taarifa za Pato la Taifa kwa robo mwaka ni kiashiria ambacho hutumika kutathmini mabadiliko ya kiuchumi katika vipindi vifupi na kuwezesha kutayarisha sera za kiuchumi kwa wakati muafaka katika Nchi.

1.1 Uchumi wa Dunia

Uchumi wa Dunia unatarajiwa kukua kwa asilimia 6.0 mwaka 2021 ikilinganishwa na ukuaji wa kiwango hasi cha asilimia 3.3 mwaka 2020. Kiwango kizuri cha ukuaji kinatarajiwa katika mwaka 2021 baada ya kuanza kwa janga la ugonjwa wa UVIKO-19. Kiwango hiki kitatokana na nchi mbalimbali kuendelea kuchukua hatua za kuweka vizuizi vya kusafiri nje, kutumia njia mbadala za kufanya kazi, misaada ya kibajeti kwa baadhi ya nchi zenyenye uchumi mkubwa Duniani kupunguza athari za UVIKO-19 kutokana na matumizi ya chanjo katika nusu ya pili ya mwaka 2021 hatua amabazo zinatarajiwa kuimarisha ukuaji wa uchumi. Athari kubwa za ajira na mapato zimeonekana mionganini mwa makundi ya vijana, wanawake, wafanyakazi wenye viwango vidogo vya elimu na kwa waliojiajiri katika sekta isiyo rasmi. Aidha, nchi zinazotegemea shughuli za utalii na uuzaaji wa bidhaa nje ya nchi na ambazo hazikuwa misaada ya kibajeti kujinusuru kutokana na janga la UVIKO-19 zimeathirika kwa kiasi kikubwa.

1.2 Uchumi wa Nchi Zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara


Nchi zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara ziliathirika zaidi mwaka 2020 kutokana na Janga la UVIKO-19 ambapo uchumi katika eneo hili ulikua kwa kiwango hasi cha asilimia 1.9. Aidha, uchumi katika eneo hili unatarajiwa kuimarika na kukua kwa asilimia 3.4 mwaka 2021. Nchi zilizo katika eneo hili zinazotegemea utalii ziliathirika zaidi katika mwaka 2020 kutokana na hatua za nchi mbalimbali kuendelea kuweka vizuizi vya kusafiri nje ya nchi. Athari zake zinaonekana kwa nchi zinazotegema zaidi utalii ambapo idadi ya watalii imepungua na hivyo kuathiri ukuaji wa uchumi.

1.3 Uchumi wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika

Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) zilishuhudia kuathirika kwa uchumi kutokana na athari za UVIKO-19 tangu ulipoanza na baada ya kipi ndi

hicho. Katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Machi 2021, uchumi kwa baadhi ya nchi uliathirika zaidi ambapo uliongezeka kwa kiwango hasi cha asilimia 1.0 ikilinganishwa na kiwango hasi cha asilimia 0.3 kipindi kama hicho mwaka 2020 (Kielelezo 1).


Kielelezo 1: Ukuaji wa Uchumi Katika Nchi za SADC - Robo ya Kwanza, Mwaka 2021



1.4 Ukuaji wa Uchumi Katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki

Ukuaji wa uchumi mionganoni mwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kipindi cha robo ya kwanza mwaka 2021 ulionyesha kuwa: uchumi wa Rwanda uliongezeka kwa asilimia 3.5 ikilinganishwa na asilimia 3.7 mwaka 2020, wakati uchumi wa Tanzania ulikua kwa asilimia 4.9 katika robo ya kwanza ya mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 5.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2020 na uchumi wa Uganda ulikua kwa asilimia 6.2 katika robo ya kwanza ya mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 0.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Nchi za Kenya, Burundi na Sudani Kusini haujatolewa.

Kielelezo 2: Ukuaji wa Uchumi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Robo ya Kwanza Mwaka 2016 – 2021



1.5 Ukuaji wa Uchumi Nchini Tanzania

Muhtasari huu unahu su taarifa za awali za Pato la Taifa kwa bei za miaka husika na bei za mwaka wa kizio wa 2015 kwa Tanzania Bara

Taarifa zilizokusanywa kutoka katika shughuli zote za uzalishaji wa bidhaa na huduma zilitumika kutayarisha takwimu za Pato la Taifa Robo ya Kwanza (Januari - Machi) ya Mwaka 2021. Halikadhalika, ukokotoaji umezingatia matakwa ya Mfumo wa Umoja wa Mataifa wa Kutayarisha Takwimu za Pato la Taifa unaojulikana kama *System of National Accounts 2008*. Muhtasari huu unatoa matokeo ya Pato la Taifa kwa bei za miaka husika na Pato la Taifa kwa bei za mwaka wa kizio wa 2015.


Aidha, Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilianza kutekeleza Sera ya Marekebisho ya Takwimu za Pato la Taifa mwanzoni mwa mwaka 2019. Sera hii inaruhusu kuchapisha matokeo ambayo yanaweza kufanyiwa marekebisho kutokana na upatikanaji wa takwimu mpya za kila robo mwaka na za kila mwaka.

1.5.1 Ukuaji wa Uchumi Katika Robo ya Kwanza, Mwaka 2021

Katika kipindi cha robo ya Kwanza (Januari - Machi) ya mwaka 2021, thamani ya Pato la Taifa kwa bei za miaka husika iliongezeka hadi shilingi trilioni 38.0 kutoka shilingi trilioni 36.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Vile vile, thamani ya Pato la Taifa kwa bei za mwaka 2015 iliongezeka hadi shilingi trilioni 33.2 katika robo ya kwanza ya mwaka 2021 kutoka shilingi trilioni 31.7 katika kipindi kama

hicho mwaka 2020 sawa na ukuaji wa asilimia 4.9. Aidha, ukuaji wa uchumi katika mwaka 2021 unakadiriwa kufikia asilimia 5.7.


Kielelezo 3: Kasi ya Ukuaji wa Pato la Taifa, Robo ya Kwanza Mwaka 2015 – 2021



1.5.2 Mchango wa Shughuli Kuu za Uchumi, Robo ya Kwanza, Mwaka 2021

Mchango wa shughuli za kiuchumi kwa kuzingatia mchanganuo wa shughuli kuu za kiuchumi za msingi (*primary activities*), shughuli za kati (*secondary activities*) na shughuli za huduma (*tertiary activities*) unaonesha kuwa: shughuli za Huduma zilichangia asilimia 40.1 ya Pato la Taifa zikifua tiwa na shughuli za Msingi zilichangia asilimia 37.1 na shughuli za kati zilichangia asilimia 22.7. Mchango umekokotolewa kabla ya kujumuisha mchango wa kodi.


Kielelezo 4: Mchango wa Shughuli Kuu za Kiuchumi, Robo ya Kwanza Mwaka 2021



1.5.3 Viwango vya Ukuaji wa Shughuli za Kiuchumi, Januari Machi 2021

Katika kipindi cha Januari hadi Machi 2021, shughuli ya uchumi ya Uchimbaji wa Madini na Mawe iliongoza kwa kuwa na kiwango cha juu cha ukuaji wa asilimia 10.2 ikifuatiwa na Habari na Mawasiliano asilimia 9.1. Shughuli ya Uchukuzi na Uhifadhi Mizigo; na Shughuli za Maji safi na Maji taka kila moja ziliongezeka kwa asilimia 9.0. Aidha, Shughuli ya Kitalaam, Sayansi na Ufundu iliongezeka kwa asilimia 7.8, Shughuli ya Huduma zinazohusiana na Utawala iliongezeka kwa asilimia 7.4, na Shughuli ya Umeme iliongezeka kwa asilimia 7.2.

Kielelezo 5: Ukuaji wa Shughuli za Uchumi - Robo ya Kwanza, Mwaka 2021



1.5.4 Mchango Katika Ukuaji wa Uchumi, Robo ya Kwanza, Mwaka 2021

Ukuaji wa Pato la Taifa katika robo ya kwanza ya mwaka 2021 ulikuwa wa asilimia 4.9. Ukuaji huu ulichangiwa na shughuli zote za kiuchumi zilizofanyika Nchini katika kipindi hicho. Aidha, mchango mkubwa katika ukuaji ulichangiwa kutoka katika shughuli za kiuchumi za: Ujenzi kwa asilimia 14.9, Uchukuzi na Uhifadhi wa Mizigo kwa asilimia 14.6; Kilimo kwa silimia 12.7, Uzalishaji Viwandani kwa asilimia 9.8 na Uchimbaji wa Madini na Mawe kwa asilimia 8.8.

2.0 Ukuaji wa Shughuli za Uchumi

Shughuli za kiuchumi zilizochangia katika ukuaji wa uchumi kwa asilimia 4.9 katika robo ya kwanza ya mwaka 2021 ni kutoka katika shughuli za Msingi, za kati na za Huduma. Baadhi ya shughuli za kiuchumi zimefafanuliwa kwa kina kama ifuatavyo:

2.1 Kilimo, Misitu na Uvuvu


Shughuli hizi zinahusika na uvunaji wa rasilimali za asili za mboga za majani na wanyama zinazojumuisha mazao ya kupandwa, ufugaji na uzalishaji wa wanyama, uvunaji wa miti na mimea mingine, wanyama au bidhaa za wanyama kutoka katika mashamba ya ufugaji au mazingira ya asili.

2.1.1 Mazao

Mazao makuu yaliyojumuishwa ni pamoja na mahindi, mpunga, ulezi/mtama, nafaka nyagine, mihogo, viazi mviringo, viazi vitamu, maharagwe, mikunde, mbegu za mafuta, mboga mboga, ndizi, matunda mengine, karanga, kahawa, pamba, chai, tumbaku na mazao mengine ya chakula na biashara.

Shughuli ya uzalishaji wa mazao iliongezeka kwa kiwango kidogo cha asilimia 1.6 katika kipindi cha robo ya kwanza ya 2021 ikilinganishwa na asilimia 3.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Ukuaji wa shughuli ya mazao ultokana na upatikanaji wa mvua juu ya wastani iliyoababisha kupungua kwa uzalishaji wa mazao katika baadhi ya maeneo ya uzalishaji.

Kielelezo 6: Uzalishaji wa Baadhi ya Mazao, Robo ya Kwanza Mwaka 2020 – 2021



Baadhi ya mazao yaliyochangia ukuaji wa shughuli ya mazao katika robo ya kwanza ya mwaka 2021 yalikuwa kama ifuatavyo: mahindi yaliongezeka kwa asilimia 2.2 kutoka tani milioni 2.734 mwaka 2020 hadi tani milioni 2.794 mwaka 2021; mpunga uliongezeka kwa asilimia 9.6 kutoka tani elfu 424 mwaka 2020 hadi tani elfu 465 mwaka 2021. Mazao mengine yalikuwa viazi vitamu vilivyoongezeka kwa asilimia 7.2 kutoka tani elfu 319 mwaka 2020 hadi tani elfu 342 mwaka 2021; mtama iliongezeka kwa asilimia 16.2 kutoka tani elfu 341 mwaka 2020 hadi tani elfu 396 mwaka 2021; maharage na mazao jamii ya mikunde yaliyoongezeka kwa asilimia 6.9 kutoka tani elfu 156 mwaka 2020 hadi tani elfu 167 mwaka 2021 na Ngano iliongezeka kwa asilimia 1.4 kutoka tani 26 mwaka 2020 hadi tani 27 mwaka 2021.

2.1.2 Mifugo

Shughuli hii inahusika na ufugaji ng'ombe wa asili na wa kisasa, mbuzi; kondoo; punda, farasi; nguruwe, sungura, kuku wa kienyeji na kisasa; na ndege wa aina nyingine.

Shughuli ya mifugo iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.0 katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2021 ikilinganishwa na kiwango cha ukuaji wa asilimia 4.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Kiwango cha ukuaji kilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa za mifugo ambayo yaliongezeka kwa kiasi kikubwa kutoptera na kuongezeka kwa pato la wastani la mwananchi, kupanuka kwa miji, pamoja na kuongezeka kwa uelewa wa wananchi kuhusu lishe bora.

2.1.3 Misitu

Shughuli hii inahusisha uzalishaji na uvunaji wa mazao ya misitu kama vile magogo, mkaa, kuni, matawi ya mti, na bidhaa nyingine zisizo za miti kama asali na nta.

Shughuli ya misitu ilikua kwa kiwango kidogo cha asilimia 0.5 katika robo ya kwanza ya mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 7.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Ukuaji huo ultokana na kuongezeka kwa usimamizi wa rasilimali za misitu na pia juhudini za Serikali kuhakikisha uvunaji endelevu wa bidhaa za misitu.

2.1.4 Uvuvi

Shughuli ya uvuvi inahusika na uvunaji wa rasilimali za uvuvi katika maji ya bahari na vyanzo vingine vya maji baridi.

Shughuli hii ilikua kwa kiwango hasi cha asilimia 0.6 katika robo ya kwanza ya mwaka 2021 ikilinganishwa na kiwango cha ukuaji wa asilimia 0.1 katika robo ya kwanza ya mwaka 2020. Kiwango cha ukuaji kilitokana na kupungua kwa uvunaji samaki na mazao yake.

2.2 Uchimbaji wa Madini na Mawe

Shughuli ya uchimbaji wa Madini na Mawe inahusisha madini yabisi kama vile makaa ya mawe, vimiminika (petroli) au gesi (gesi asilia). Uchimbaji wa madini na mawe hufanyika chini ya ardhi, ukusanyaji juu ya ardhi au kwenye visima. Pia inajumuisha shughuli za ziada zinazolenga kutayarisha madini kwa ajili ya kuuzwa, kwa mfano, kusaga, kusafisha na kukausha. Shughuli hizi mara nyingi zinafanywa na vitengo ambavyo vinavuna rasilimali za madini / au nyingine zilizopo karibu na migodi.

Shughuli ya uchimbaji wa madini na mawe imegawanyika katika maeneo makuu manne ambavyo ni:

- 1) Madini ya makaa ya mawe;
- 2) Petroli na gesi asilia;
- 3) Uchimbaji wa madini ya chuma; na
- 4) Madini ya kokoto na mawe

Shughuli ya uchimbaji wa madini na mawe iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 10.2 katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 15.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Ukuaji ulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa madini ya dhahabu, Makaa ya mawe na jasi. Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2021, uzalishaji wa dhahabu uliongezeka hadi tani 14,504.42 kutoka kilo 12,404.32 kipindi kama hicho mwaka 2020.

Jedwali Na 1: Uzalishaji wa Madini, Robo ya Kwanza Mwaka 2016 – 2021

Madini	Kipimo	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Dhahabu	kilo	10,596	10,699	8,655	8,656	12,404	14,504
Makaa ya Mawe	Tani	38,704	128,712	129,873	205,045	160,855	190,932
Jasi	Tani	44,077	23,125	50,594	75,593	72,390	140,376
Gesi Asilia	Futa za Ujazo Milioni	11,980	12,710	13,729	16,138	14,573	16,090

2.3 Viwanda

Shughuli ya uzalishaji viwandani inahusisha uchakataji wa bidhaa kutoka katika hali yake ya kawaida na kuzalisha bidhaa za aina nyingine ambazo zinaweza kutumika moja kwa moja na mlaji wa mwisho au kutumika kuzalisha bidhaa nyingine. Bidhaa zinazoweza kuchakatwa ni pamoja na bidhaa za kilimo, misitu, uvuvi, madini na bidhaa nyingine za viwandani.

Shughuli ya uzalishaji viwandani iliongezeka kwa kasi ya asilimia 6.3 katika robo ya kwanza ya mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 4.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Kiwango cha ukuaji kilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za viwandani kwa ujumla.

2.4 Umeme

Shughuli hii inahusika na uzalishaji na usambazaji wa umeme na gesi asilia, kupitia miundombinu ya kudumu ya waya na mabomba. Uzalishaji wa umeme ni kutoka katika vyanzo vya maji, mafuta na gesi. Pia inahusika na shughuli za usambazaji na ugawaji wa umeme. Vyanzo vikuu vya takwimu za uzalishaji wa umeme ni kutoka katika makampuni ya uzalishaji wa umeme.

Katika kipindi cha Januari hadi Machi 2021, shughuli hii iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 7.2 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.2 katika robo ya kwanza ya mwaka 2020. Kiasi cha umeme uliozalishwa kilikuwa saa za kilowati milioni 2,036 mwaka 2021 ikilinganishwa na saa za kilowati milioni 1,976 katika kipindi kama hicho mwaka 2020.

2.5 Maji Safi na Maji Taka

Shughuli hii inahusika na kukusanya na kusafisha maji kwa ajili ya ugavi wa maji, kusafisha maji ya bahari kwa kuondoa chumvi ili kuweza kuzalisha maji ya kutumia kama bidhaa kuu na kukusanya maji moja kwa moja kutoka katika visima kwa ajili ya matumizi ya makampuni ya maji au matumizi binafsi katika kilimo au kaya. Aidha, shughuli hii pia inahusika na ukusanyaji wa maji taka.

Katika kipindi cha Januari hadi Machi 2021, kiasi cha maji kilichozalishwa kilikuwa mita za ujazo milioni 76.8 ikilinganishwa na mita za ujazo milioni 69.8 zilizozalishwa

kipindi kama hicho mwaka 202. Shughuli hii ilikua kwa kiwango cha asilimia 9.0 katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 7.2 kipindi kama hicho mwaka 2020. Ukuaji huu ilitokana na kuendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji pamoja na uboreshaji wa miundombinu ya kuzalisha na kusambaza maji nchini.

Kielelezo 7: Maji yaliyozalishwa (Mita za Ujazo Milioni), Robo ya kwanza, Mwaka 2017 – 2021



2.6 Ujenzi

Shughuli hii inajumuisha ujenzi wa aina zote na shughuli maalum za ujenzi kwa ajili ya majengo na kazi za uhandisi. Shughuli hii inajumuisha pia ujenzi mpya, ukarabati, kufanya mabadiliko makubwa kwenye majengo na ujenzi wa miundombinu.

Ujenzi wa aina zote unajumuisha ujenzi wa nyumba nzima, majengo ya biashara/ofisi, maduka na majengo mengine ya umma na miundombinu ya mashambani. Ujenzi pia unajumuisha ujenzi wa barabara, madaraja, reli, viwanja vya ndege, bandari na miundombinu ya maji, mifumo ya umwagiliaji, mifumo ya majitaka, miundombinu ya viwanda, mabomba na mifumo ya umeme na vituo vya michezo.

Shughuli ya ujenzi iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.2 katika robo ya kwanza ya mwaka 2021, ikilinganishwa na asilimia 4.9 katika robo ya kwanza ya mwaka 2020. Ukuaji ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa ndani wa vifaa vya ujenzi

kama saruji, chuma na vyuma ambavyo ni viashiria vinavyotumika kutathmini ongezeko la thamani la shughuli ya ujenzi.

2.7 Biashara na Matengenezo

Shughuli hii inajumuisha uuzaji wa jumla na rejareja (uuzaji wa bidhaa bila ya kufanya mabadiliko) wa aina yoyote ya bidhaa, pamoja na utoaji wa huduma kwa ajili ya uuzaji wa bidhaa. Pia inahusisha ukarabati wa magari na usimikaji wa mitambo na ukarabati wa bidhaa za binafsi na za nyumbani. Shughuli kuu ni kununua na kuuza bidhaa.

Shughuli ya uuzaji wa bidhaa wa jumla na rejareja iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 4.6 katika robo ya kwanza ya mwaka 2021 ikilinganishwa na kiwango cha ukuaji wa asilimia 4.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Ukuaji huo ulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa kwa ajili ya kuuzwa hususan bidhaa za viwandani.

2.8 Uchukuzi na Uhifadhi wa Mzigo

Shughuli hii inahusisha utoaji wa huduma ya usafiri wa abiria au/na mizigo, ikiwa ni kwa ratiba maalum au isiyokuwa na ratiba, kwa njia ya reli, bomba, barabara, maji au anga na shughuli zinazohusiana ikiwa ni pamoja na utunzaji wa mizigo na uhifadhi. Shughuli hii pia inajumuisha kukodisha vifaa vya usafiri na madereva na shughuli za posta na usafirishaji wa vifurushi.

Shughuli ya usafirishaji na uhifadhi wa mizigo iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 9.0 katika robo ya kwanza ya mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 8.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Kiwango cha ukuaji kilitokana na kuongezeka kwa idadi ya abiria na mizigo iliyosafirishwa katika kipindi hicho hususan kwa upande wa usafirishaji wa mizigo kwa njia ya barabara.

2.9 Malazi na Huduma ya Chakula

Shughuli hii inajumuisha utoaji huduma ya makazi ya muda mfupi kwa wageni na wasafiri wengine na utoaji wa huduma ya chakula na vinywaji kwa mlaji wa mwisho.

Huduma ya malazi na chakula iliongezeka kwa kiwango hasi cha asilimia 6.5 katika robo ya kwanza ya mwaka 2021 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 2.6 katika


mwaka 2020. Ukuaji huo ulitokana na kupungua kwa idadi ya watalii na vitanda vilivyotumika kulala wageni kulikotokana na hatua za kufungia wananchi ili kudhibiti kusambaa kwa UVIKO-19 katika nchi wanazotoka watalii katika kipindi hicho. Katika kipindi hicho, idadi ya watalii walikuwa 231,131 ikilinganishwa na watalii 336,510 katika robo ya kwanza ya mwaka 2020.

2.10 Habari na Mawasiliano

Shughuli hii inahusika na uchapishaji, upigaji picha za kawaida, picha za video na uzalishaji wa programu za televisheni, kurekodi sauti na kuchapisha muziki, shughuli za programu na utangazaji, kwa mfano, utangazaji wa redio na televisheni, mawasiliano ya simu, programu za kompyuta, ushauri na shughuli zinazohusiana na shughuli za huduma za habari kama vile uchakataji wa data.

Shughuli hii iliongezeka kwa asilimia 9.1 katika robo ya kwanza ya mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 8.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Kiwango cha ukuaji kilitokana na kuongezeka kwa muda wa maongezi uliotumiwa na wateja wa simu za mkononi na upanuzi wa huduma za utangazaji na mtandao.

Kielelezo 8: Mauzo ya Huduma za Mawasiliano, Robo ya kwanza Mwaka 2017 – 2021




2.11 Fedha na Bima

Shughuli hii inahusika na utoaji wa huduma za fedha, bima, pensheni ya hiari, na huduma nyingine za fedha.

Shughuli ya fedha na bima ilikua kwa kiwango cha asilimia 4.3 katika robo ya kwanza ya mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 4.1 katika robo ya kwanza ya

mwaka 2020. Ukuaji ulitokana na kuongezeka kwa amana kwa asilimia 5.4 kutoka shilingi trilioni 21.9 katika robo ya kwanza ya mwaka 2020 hadi shilingi trilioni 23.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Aidha, mikopo iliongezeka kwa asilimia 2.7 kutoka shilingi trilioni 19.4 katika robo ya kwanza ya mwaka 2020 hadi shilingi trilioni 20.0 katika robo ya kwanza ya mwaka 2021; na pia kuongezeka kwa huduma zinazotolewa na makampuni ya bima.

Kielelezo 9: Mikopo na Amana za Benki, Robo ya Kwanza Mwaka 2016 – 2021



2.12 Upangishaji Majengo

Shughuli hii inahusika na utoaji wa huduma za kuuza au kununua majengo, kukodisha mali, majengo na pia kutoa huduma nyingine za mali isiyohamishika ikiwa ni pamoja na kupima mali isiyohamishika kama vile viwanja.

Kiwango cha ukuaji kilikuwa asilimia 4.6 katika robo ya kwanza ya mwaka 2021 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.5 kipindi kama hicho mwaka 2020. Ukuaji ulitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya nyumba za kuishi na biashara hususan katika maeneo ya mijini.

2.13 Shughuli za Kitalaam, Sayansi na Ufundı

Shughuli hii inajumuisha shughuli maalum za kitalaam, kisayansi na kiufundi. Shughuli hizi zinahitaji kiwango cha juu cha mafunzo, pamoja na kupata ujuzi maalum unaotumika kutoa huduma kwa watumiaji.

Shughuli hii inahusisha huduma za kisheria na uhasibu; ushauri na usimamizi; usanifu na uhandisi; kupima na uchambuzi wa kitaalam; utafiti wa kisayansi na maendeleo; matangazo na utafiti wa masoko; utaalamu wa aina nyingine wa kisayansi na kiufundi pamoja na shughuli za ugani.

Shughuli hii iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 7.8 katika robo ya kwanza ya mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 8.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Kiwango cha ukuaji kilitokana na ongezeko la mahitaji ya shughuli za kitaaluma, kisheria na kiuhasibu.

2.14 Huduma Zinazohusiana na Utawala

Shughuli hii inajumuisha huduma mbalimbali zinazosaidia kufanyika kwa biashara. Shughuli inajumuisha huduma za kukodisha vifaa, ajira, huduma za uwakala wa kampuni za usafiri, huduma za kuongoza watalii, huduma za kuandaa malazi; na huduma nyingine zinazohusiana na usalama na uchunguzi; pamoja na huduma kwenye majengo na uboreshaji wa mazingira.

Kiwango cha ukuaji kiliongezeka kwa asilimia 7.4 katika robo ya kwanza ya mwaka 2021 ikilinganishwa na kiwango cha ukuaji wa asilimia 8.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2020.

2.15 Utawala na Ulinzi

Shughuli ya utawala na ulinzi inahusika na kutunga na kutafsiri sheria, kukusanya kodi, ulinzi wa mipaka ya nchi, usalama wa raia na mali zao, huduma za uhamiaji, pamoja na uendeshaji wa serikali kwa ujumla. Aidha, huduma za mifuko ya lazima ya hifadhi ya jamii inajumuishwa katika shughuli hii.

Shughuli hii iliongezeka kwa asilimia 2.3 katika robo ya kwanza ya mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 5.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Ukuaji ulitokana na kuongezeka kwa matumizi ya Serikali katika sekta za jamii na katika kutoa huduma za utawala na ulinzi.

2.16 Elimu

Shughuli hii inajumuisha utoaji wa elimu katika ngazi zote, kwa njia ya kuongea au maandishi au kwa njia ya redio na televisheni au njia nyingine za mawasiliano. Inajumuisha elimu inayotolewa na taasisi tofauti katika mfumo wa kawaida wa shule katika ngazi tofauti tofauti pamoja na elimu ya watu wazima na elimu ya kujifunza kusoma na kuandika. Shughuli hii inajumuisha elimu katika sekta ya umma na binafsi.

Shughuli hii ilikua kwa kiwango cha asilimia 4.9 katika robo ya kwanza ya mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 5.4 katika robo ya kwanza ya mwaka 2020. Ukuaji ulitokana na ongezeko la idadi ya wanafunzi walioandikishwa katika shule za msingi na sekondari.

2.17 Afya na Huduma za Jamii

Shughuli hii inajumuisha utoaji wa huduma za afya na maendeleo ya jamii. Inajumuisha huduma za afya zinazotolewa na wataalam wa matibabu katika hospitali na vituo vingine, shughuli nyingine za huduma za makazi ambazo zinahusisha shughuli za huduma za afya kwa jamii bila ushirikishwaji wa wataalamu wa huduma za afya.

Shughuli hii ilikua kwa kiwango cha asilimia 4.2 katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2021 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 9.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Ukuaji ulitokana na kuongezeka kwa idadi ya wagonjwa waliohudumiwa katika vituo vya afya vya binafsi.

2.18 Sanaa na Burudani

Shughuli hii inajumuisha shughuli mbalimbali zinazotolewa ili kukidhi maslahi mbalimbali ya kitamaduni na utoaji wa burudani kwa umma kwa ujumla. Shughuli hii pia inahusika na burudani za bendi, uendeshaji wa maeneo ya makumbusho, kamari, shughuli za huduma michezo na burudani kwa ujumla.

Ukuaji wa shughuli ya Sanaa na Burudani iliongezeka kwa kiwango hasi cha asilimia 5.3 katika robo ya kwanza ya mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 11.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Kupungua kwa kasi ya ukuaji kilitokana na kupungua kwa mauzo ya bidhaa za kitamaduni kwa watalii kulikosababishwa na kupungua kwa watalii walitembelea vivutio mbalimbali katika kipindi husika.

2.19 Huduma Nyingine za Kijamii

Shughuli hii inajumuisha shughuli za mashirika ya uanachama, ukarabati wa vifaa vyakielettroniki na bidhaa za kibinafsi za nyumbani na shughuli mbalimbali za huduma za binafsi ambazo hazijumuishwi kwenye shughuli nyingine.

Shughuli hii iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 7.8 katika robo ya kwanza ya mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 6.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Ukuaji wa shughuli hii ulitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya huduma za kijamii katika kipindi hicho.

2.20 Shughuli za Kaya katika Kuajiri

Shughuli za kaya kama mwajiri zinajumuisha wafanyakazi wa ndani kama vile wajakazi, wapishi, wahudumu, wafugaji, watengenezaji wa bustani, wakulima, walini wa mlangoni, madereva wa magari, waangalizi wa watoto, wafundishaji na masekretari. Bidhaa na huduma zinazozalishwa na shughuli hii hutumiwa na kaya inayoajiri.

Shughuli hii iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 3.1 katika robo ya kwanza ya mwaka 2021 sawa na ilivyokuwa katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Kiwango cha ukuaji kilitokana na ongezeko la wakazi wa mijini.

3.0 Hitimisho

Takwimu za Pato la Taifa kwa robo mwaka hutumika kupima shughuli za kiuchumi katika vipindi vifupi vyakielettroniki na bidhaa za kijamii. Kiwango cha ukuaji wa uchumi katika kipindi cha robo ya kwanza (Januari – Machi) ya mwaka 2021 kiliongezeka kwa asilimia 4.9

ikilinganishwa na asilimia 5.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Katika kipindi hicho kasi ya ukuaji wa shughuli za uchumi zilichangiwa na shughuli mbalimbali za kiuchumi zikiwa ni pamoja na Uchimbaji wa Madini na Mawe kwa asilimia 10.2, Habari na Mawasiliano asilimia 9.1, Uchukuzi na Uhifadhi Mizigo asilimia 9.0, Maji safi na maji taka 9.0, shughuli za Kitalaam, Sayansi na Ufundu asilimia 7.8, shughuli za huduma zinazohusiana na Utawala asilimia 7.4 na shughuli ya Umeme 7.2.

Kiambatisho Na.1: Pato la Taifa kwa Shughuli za kiuchumi kwa Bei za Mwaka 2015 – Sh. Milioni

Mwaka	Robo mwaka	kilimo	Madini na Mawe	Viwanda	Umeme	Maji safi na maji taka	Ujenzi	Biasara na Matengenezo	Malazi na Huduma ya Chakula	Uchukuzi na Uhifadhi Mizigo	Habari na Mawasiliano	Fedha na Bima	
2012		21,807,030	3,314,742	6,066,989	669,069	358,361	7,578,263	7,371,411	1,343,924	5,710,466	1,266,747	3,444,161	
2013		22,408,192	3,464,721	6,292,514	723,608	367,890	9,023,353	7,682,286	1,356,204	6,050,976	1,414,116	3,405,940	
2014		23,952,077	3,687,273	6,919,794	815,297	381,760	9,253,082	8,444,243	1,397,782	6,577,706	1,560,064	3,764,113	
2015		25,234,560	4,055,619	7,411,672	798,801	390,758	10,446,797	8,747,862	1,421,916	6,929,895	1,681,098	4,189,021	
2016		26,436,338	4,356,709	8,213,364	869,262	417,899	11,960,720	9,260,703	1,480,052	7,324,856	1,718,548	4,235,515	
2017		28,008,976	4,588,624	8,889,818	877,667	444,660	13,765,005	9,821,248	1,525,619	7,815,845	1,824,471	4,115,393	
2018		29,504,198	4,659,195	9,623,501	928,174	477,510	15,655,747	10,396,691	1,604,391	8,736,561	1,989,717	4,094,972	
2019		30,802,027	5,485,112	10,184,558	994,879	510,411	17,802,021	10,965,038	1,645,950	9,493,191	2,133,312	4,281,167	
2020		32,321,327	5,850,231	10,646,279	1,049,611	540,159	19,421,672	11,194,534	1,419,654	10,293,276	2,313,033	4,412,967	
		1	5,994,220	748,412	1,459,422	167,460	87,306	2,146,785	1,828,162	332,454	1,519,508	312,238	811,387
2013		2	5,376,452	850,463	1,547,040	177,004	90,069	2,111,891	1,884,307	324,659	1,501,581	343,060	836,571
		3	4,199,755	875,290	1,677,731	181,477	85,918	2,389,873	1,893,295	354,104	1,513,039	358,452	881,698
		4	6,837,765	990,556	1,608,322	197,667	104,598	2,374,804	2,076,522	344,987	1,516,849	400,366	876,284
		1	6,335,448	937,448	1,621,405	201,849	87,893	2,182,230	2,054,479	346,623	1,625,429	342,909	912,095
2014		2	5,877,120	871,899	1,706,772	182,845	94,708	2,507,336	2,073,942	339,327	1,616,710	380,305	927,895
